COMPETENCY BASED CURRICULUM SHUGHULI ZA KISWAHILI - GRADE 2 EXAMS TERM 1 2023

Maswali

SEHEMU YA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

1. Familia yako ina watu wangapi?
2. Je, wewe na familia yako mnaishi wapi?
3. Ni nani huwapikia katika familia yako?
4. Je, unaye ndugu yeyote katika familia yako?
5. Wewe husaidiaje katika familia yako ukiwa nyumbani?

SEHEMU YA 2: KUSOMA

Zoezi la 1: Kusoma kwa sauti.

Jioni moja, mama alikuja nyumbani akiwa na furaha nyingi. Aliniambia kuwa baba angesafiri kuja nyumbani siku iliyofuata. Niliposikia hivyo, nilirukaruka kwa furaha.

Zoezi la 2: Kusoma kwa Ufahamu.

Soma hadithi na ujibu maswali yafuatayo.

Sami na Kiki ni marafiki wakubwa. Wao wanapendana sana. Wao ni wanafunzi wa gredi ya pili katika shule ya Mamboleo. Mwalimu wao anaitwa Bi. Rukia. Mwalimu huyo hufundisha kwa bidii sana. Wanafunzi wake humpenda kwa sababu bidii yake kazini. Siku zote, yeye huwaambia kuwa wafanye bidii kwa sababu bidii hulipa.

11. Sami na Kiki wanasoma katika shule ya.....
12. Mwalimu aliyetajwa anaitwa Bi.....
13. Wanafunzi humpenda mwalimu wao kwa sababu ya.....
14. Sami na Kiki ni wanafunzi wa gredi ya.....
15. Siku zote, mwalimu huyo huwaambia wanafunzi wake kuwa.....

SEHEMU YA 3: SARUFI

Chagua jibu sahihi kutoka mabononi.

16. Mwanafunzi ameketi.....ya mwalimu wake. (katikati, ndani, mbele)
17. Mafuta yamo..... ya chupa. (ndani, juu, katikati)
18. Paka amekaa.....yameza na kiti,(chini, ndani, katika)
19. Wageni wameingia.....ya nyumba. (juu, ndani, nje)

Jaza Jedwali hili kwa usahihi.